# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA AROBAINI NA TANO

**12 JUNI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA AROBAINI NA TANO - TAREHE 12 JUNI, 2025

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### WAZIRI WA FEDHA:

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 *(Monetary Policy Statement for the Year 2025/2026).*

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**576 MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (NKASI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Stendi ya kisasa na kuweka Taa za Barabarani Namanyere - Nkasi.

**577 MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati mkubwa wa Soko la Mbagala Kizuiani.

## OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

**578 MHESHIMIWA SOUD MOHAMED JUMAH (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kuna mkakati gani kuimarisha uhifadhi wa mazingira ya Mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere ili kuhakikisha uendelevu wa Mradi huo .

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**579 MHESHIMIWA VINCENT PAUL MBOGO (NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Bwawa la Lambo la kunyweshea mifugo Kijiji cha Kacheche na ujenzi wa Josho Nyikankulu Kata ya Chala – Nkasi Kusini.

**WIZARA YA UJENZI:**

**580 MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Mlowo - Kamsamba utaanza.

**WIZARA YA MAJI:**

**581 MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Maji Kata ya Songambele - Kyerwa.

**582 MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Visima vilivyochimbwa katika Kata za Mlingula, Mkwapa na Namatutwe - Masasi vitawekwa pampu.

**583 MHESHIMIWA BAHATI KENETH NDINGO (MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, nini mkakati wa Serikali kusaidia upatikanaji wa maji safi na salama Mbarali kutoka asilimia 58 kufikia lengo la Serikali la asilimia 85.

**WIZARA YA AFYA:**

**584 MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti ongezeko la Wagonjwa wa Kansa nchini.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**SAA 10:00 ALASIRI**

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**DODOMA**
**12 JUNI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**